TANGAZO LA SERIKALI Na. 29 la tarehe 12/1/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 6(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA IRINGA YA MWAKA 2023

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Manispaa ya Iringa ya Mwaka 2023.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Manispaa ya Iringa.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Iringa;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

"madini ya ujenzi" maana yake ni tarazo, moramu, udongo, kifusi, kokoto, mawe, mchanga, chokaa na madini mengine yanayotumika katika ujenzi;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa au Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"soko" maana yake ni eneo lililotengwa na linalomilikiwa na Halmashauri kama soko;

"stendi" maana yake ni eneo maalumu lililotengwa au kujengwa na Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria au mizigo hii itajumuisha pia kituo cha kupaki malori na vituo vingine vidogo vidogo vya kupakia na kushusha abiria vya Halmashauri;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"utamaduni" inajumuisha sanaa za maonyesho, sanaa za ufundi, muziki wa asili, ususi, michezo, disko, muziki wa dansi, picha mjongeo, muziki wa taarabu, maonyesho ya sinema, mazingaombwe, tiba za jadi na matumizi ya viwanja vya michezo;

"vyombo vya moto" maana yake ni magari, mitambo na pikipiki za aina zote; na

"wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni iliyoteuliwa kukusanya ada na ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

Utozaji wa ada na ushuru

4.-(1) Halmashauri itatoza ada na ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Ada au ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au wakala wa Halmashauri kama Halmashauri itakavyoelekeza.

(3) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa kulipa ada na ushuru

5. Mtu yeyote anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atatakiwa kulipa ada au ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Muda wa kukusanya ada au ushuru

6.-(1) Muda wa kukusanya ada au ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (1), Halmashauri au wakala kwa kibali maalumu kutoka kwa

Mkurugenzi, anaweza kukusanya ada au ushuru baada ya muda uliotajwa hapo juu.

(3) Malipo ya ada au ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yeyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ada au ushuru.

Utoaji wa stakabadhi za malipo

7.-(1) Ada au ushuru utakaotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au kwa wakala ambaye atatoa stakabadhi ya kielektroniki kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

(2) Mlipa ada au ushuru atakuwa na wajibu wa kudai na kuhakiki stakabadhi ya malipo kulingana na kiasi cha fedha alicholipa.

(3) Utakuwa si utetezi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, mtu kudai kuwa amelipa ada au ushuru bila kupewa stakabadhi ya kielektroniki.

Ukusanyaji wa madeni

8.-(1) Halmashauri inaweza kukusanya ushuru kwa njia ya mahakama endapo mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni itakuwa imeshindwa kulipa ada au ushuru kwa muda uliokubaliwa.

(2) Bila kuathiri masharti yaliyoainishwa katika aya ndogo ya (1), Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ushuru kwa njia ya kukamata au kushikilia mali zinazohamishika za wadaiwa zenye thamani sawa na deni la ushuru pamoja na gharama za kukamata.

(3) Baada ya kipindi cha siku thelathini kupita tangu kukamatwa kwa mali za mdaiwa, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuziuza kwa njia ya mnada baada ya kupata idhini ya mahakama.

(4) Endapo mali zilizokamatwa zinaweza kuharibika kwa haraka, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuziuza kabla hazijaharibika baada ya kupata idhini ya mahakama.

(5) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa katika aya ndogo ya (3) na (4), kabla ya kuuza mali yoyote iliyokamatwa, Mkurugenzi atatoa taarifa ya siku saba kwa mdaiwa na umma juu ya kusudio la kuuza mali hizo.

(6) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote ile itakayotokea wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri, isipokuwa

kama hasara hiyo itakuwa imesababishwa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri au wakala.

Ushuru wa nyumba za kulala wageni

9.-(1) Kila mmiliki wa nyumba ya kulala wageni anapaswa kulipa asilimia kumi ya mapato yaliyolipwa na mgeni aliyesajiliwa.

(2) Mmiliki wa nyumba ya kulala wageni atawajibika kuwasilisha ushuru wa nyumba ya kulala wageni kila mwezi kwa Halmashauri ndani ya siku saba tangu kumalizika kwa mwezi wa malipo.

Uteuzi wa wakala

10.-(1) Halmashauri inaweza kuteua wakala kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kwa ajili ya kukusanya ada au ushuru kwa niaba yake.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa aya ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa-

(a) kukusanya na kupokea ada au ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria Ndogo hii;

(b) kukusanya ada au ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Mamlaka ya afisa mwidhiniwa

11. Bila kuathiri masharti mengine ya Sheria Ndogo hii, afisa mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni kwa nia ya kukusanya ada au ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Ulipaji wa gharama za kuhifadhi mzigo au chombo kilichokamatwa

12.-(1) Halmashauri itatoza kiasi cha asilimia tano ya thamani ya chombo kilichobeba mzigo kwa kila siku kwa mzigo ulioshikiliwa baada ya kukamatwa ukisafirishwa bila ya kulipa ada au ushuru.

(2) Chombo au mzigo husika usipokuwa umelipiwa kwa muda wa siku saba Halmashauri itauza mzigo au chombo hicho kwa njia ya mnada ili kufidia gharama zake.

Fidia ya gharama za uendeshaji wa zoezi

13. Endapo mtu anayepaswa kulipa ada au ushuru atakwepa kulipa gharama zote ambazo zitakuwa zimetumika na Halmashauri wakati wa kumkamata, mkosaji atawajibika kuzilipa.

Makosa na adhabu

14.-(1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo-

(a) atashindwa kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;
(c) atamzuia Mkurugenzi, afisa mwidhiniwa au wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(d) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au wakala kuhusu huduma zinazohitaji kulipiwa ada au ushuru;
(e) atashindwa kuweka kumbukumbu, vitabu, hesabu, au maelezo yoyote yatakayohitajika na Halmashauri;
(f) atashindwa, atadharau, atakaidi au kukataa kulipa ada au ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kuhusiana na ulipaji wa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii; au
(g) atatengeneza, atatayarisha, ataidhinisha kutengeneza au atatunza nyaraka za uongo kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa ada au ushuru ndani ya Halmashauri.

(2) Mtu atakayetiwa hatiani kwa kosa lolote chini ya Sheria Ndogo hii atatakiwa kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na kisichozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

15. Mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kiasi kisichozidi shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii.

Kufutwa kwa Sheria Ndogo TS. Na. 220 la 2018

16. Sheria Ndogo hii inafuta Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Manispaa ya Iringa ya Mwaka 2018.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(1))*

SEHEMU YA KWANZA

Ushuru wa Madini ya Ujenzi

| Namba | Aina ya madini | Kiwango cha Ada na Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Utozaji wa usombaji wa aina zote za madini ya ujenzi | 12,000/= kwa tripu<br>150,000/= kwa muda wa miezi sita<br>300,000/= kwa muda wa mwaka mmoja |
| 2. | Utoaji wa kibali cha kuchimba madini ya ujenzi | 20,000/= kwa mwaka |
| 3. | Utoaji wa kibali cha kufyatua tofari za udongo au kuchoma tanuru | 100,000/= kwa tanuru kwa mwaka |

SEHEMU YA PILI

Ada ya Kumbi na Vifaa vya Halmashauri

| Namba | | Ukodishaji wa Kumbi na Thamani | Kiwango cha Ada na Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| 1. | (i) | Ukodishaji wa kumbi za Halmashauri (Kitanzini)<br>(a) Ukumbi mkubwa<br>(b) Ukumbi mdogo | (a) 200,000/= kwa siku<br>(b) 50,000/= kwa siku |
| 2. | (ii)<br>(iii) | viti vidogo<br>viti vya chuma | 300/= kimoja kwa siku<br>500/= kimoja kwa siku |
| 3. | | Meza ndogo | 500/= kila moja kwa siku |
| 4. | | Meza kubwa | 1,000/= kila moja kwa siku |

SEHEMU YA TATU

Ushuru wa Ukaguzi wa Nyama

| Namba | Aina ya mnyama | Kiasi cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ng’ombe | 10,000/= kwa kila Ng’ombe |
| 2. | Mbuzi au kondoo | 3,000/= kwa kila Mbuzi au Kondoo |
| 3. | Nguruwe | 3,000/= kwa kila Nguruwe |
| 4. | Kuku | 200/= kwa kila kuku |

SEHEMU YA NNE

Ada ya Kuanika Ngozi

| Namba | Aina ya mnyama | Idadi ya vipande vya ngozi | Kiasi cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | kuanzia 1 hadi 1000 | 50,000/= |
| 2. | Ng'ombe | kuanzia 1000 na kuendelea | 100,000/= |
| 3. | Mbuzi na Kondoo | kuanzia 1 hadi 1000 | 25,000/= |
| 4. | Mbuzi na Kondoo | kuanzia 1000 na kuendelea | 50,000/= |

SEHEMU YA TANO

Ushuru wa Kuhifadhi Nyama

| Namba | Aina ya Mnyama | Kipimo | Kiasi cha ushuru kwa siku (Shilingi). |
|---|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | kilo 50 | 5,000/= |
| 2. | Mbuzi au Kondoo | kwa Mbuzi au kondoo | 1,000/= |

SEHEMU YA SITA

Ushuru wa Kusafirisha Mifugo nje ya Halmashauri

| Namba | Aina ya mnyama | Kiasi cha ushuru kwa siku (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 2,500/= |
| 2. | Mbuzi | 1,000/= |
| 3. | Kondoo | 1,000/= |
| 4. | Nguruwe | 1,500/= |
| 5. | Mbwa | 1,000/= |
| 6. | Paka | 1,000/= |
| 7. | Punda/Farasi | 2,500/= |
| 8. | Mayai trei 1 hadi 100 ni bure ila kuanzia trei 101 na kuendelea kila trei | 200/= kwa trei |
| 9. | Kuku ndani na nje ya Halmashauri | 200/=kwa kuku |

SEHEMU YA SABA

Ushuru wa Utumiaji wa Masoko

| Namba | Aina ya bidhaa | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa Meza | 500/= kwa siku |

SEHEMU YA NANE

Ushuru kwa matumizi ya Minada, Bidhaa na Magulio Mengine

| Namba | Aina ya Bidhaa | Kiwango cha Ada na Ushuru kwa siku (Shilingi) |
|---|---|---|

*Tangazo la Serikali Na.29 (Linaendelea.)*

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bidhaa zinazotengenezwa viwandani na karakana | 500/= |
| 2. | Wauza mitumba | 500/= |
| 3. | Wauza bia na vinywaji baridi | 500/= |
| 4. | Wauza nafaka | 500/= kwa kila gunia la kilo 100 |
| 5. | Mfugo aina ya ndege | 500/= |
| 6. | Pombe za asili | 500/= |
| 7. | Wauza madawa ya asili | 500/= |
| 8. | Wauza vipuri vya baiskeli, pikipiki, magari | 500/= |
| 9. | Wauza dagaa | 500/= |
| 10. | Wauza samaki | 500/= |
| 11. | Wauza chumvi, nyama, na mboga za majani | 500/= |
| 12. | Wauza vyungu | 500/= |
| 13. | Wauza vyombo vya nyumbani | 500/= |
| 14. | Wauza viatu | 500/= |
| 15. | Wauza nguo mpya | 500/= |
| 16. | Fundi baiskeli | 500/= |

SEHEMU YA TISA

Ada ya Ukodishaji Mitambo

| Namba | Aina ya kifaa | Kiwango cha Ada na Ushuru kwa siku (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Isuzu tipa ya tani 10 | 200,000/= |
| 2. | Isuzu tipa ya tani 7 | 150,000/= |
| 3. | Lori la mizigo tani 3.5 na kreni | 120,000/= |
| 4. | Mashine ya kuchanganyia saruji | 80,000/= |
| 5. | Mashine ya kutoa hewa kwenye sakafu | 50,000/= |
| 6. | Mashine ya kukata sehemu ngumu ya sakafu au lami iliyoharibika | 100,000/= |
| 7. | Mashine ya kusafisha barabara | 100,000/= |
| 8. | Mashine ya kuzalisha hewa | 200,000/= |
| 9. | Mashine ya mkono ya kushindilia barabara | 100,000/= |
| 10. | Mashine ya kushindilia barabara | 250,000/= |
| 11. | Mashine ya kushindilia kifusi | 70,000/= |
| 12. | Gari la kubeba maji | 150,000/= |
| 13. | Mtambo wa kumimina lami | 150,000/= |
| 14. | Mtambo wa kumimina lami kwa mkono | 200,000/= |
| 15. | Mashine ya kusambaza kukoto kwenye barabara | 200,000/= |
| 16. | Kijiko | 600,000/= |
| 17. | Greda | 800,000/= |

SEHEMU YA KUMI

Vibali vya Ujenzi

| Namba | Aina ya kibali cha ujenzi | Kiwango cha Ada na Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Viwanja vya makazi | |
| | (i) mita za mraba 0 hadi 600 | 35,000/= |

*Tangazo la Serikali Na.29 (Linaendelea.)*

| | | |
|---|---|---|
| | (ii) mita za mraba 601 hadi 1200 | 45,000/= |
| | (iii) mita za mraba 1200 na kuendelea | 55,000/= |
| | (iv) ujenzi wa nyumba zaidi ya moja | 20,000/= kwa kila nyumba itayoongezeka |
| 2. | Taasisi mbalimbali (shule, vyuo, nyumba za ibada, ofisi mbalimbali, kumbi) ambazo sio ghorofa | 200,000/= |
| 3. | Viwanda vikubwa | 300,000/= |
| 4. | Viwanda vya uzalishaji | 200,000/= |
| 5. | Viwanda vidogo | 100,000/= |
| 6. | Vituo vya mafuta | 200,000/= |
| 7. | ukarabati | 35,000/= |
| 8. | Uzio au fensi (nyumba,taasisi) | 100,000/= |
| 9. | Hifadhi ndogo, uwanja wa michezo, hoteli za utalii ambazo sio ghorofa | 200,000/= |
| 10. | Ghorofa<br>Ghorofa 1 hadi 3 | 175,000/= |
| 11. | Ghorofa 4 hadi 6 | 200,000/= |
| 12. | Ghorofa 6 na kuendelea | 200,000/= na kwa kila ghorofa inayoongezeka ni 75,000/= |
| 13. | Kuhuisha kibali cha ujenzi wa ghorofa | 200,000/= |
| 14. | Kusimika minara ya mawasiliano | 500,000/= |
| 15. | Kuhuisha kibali cha ujenzi usio wa ghorofa | Ada ni kama ilivyo kwa kibali cha awali. |

SEHEMU YA KUMI NA MOJA

Ada na Ushuru wa Maegesho

| Namba | Aina ya Gari | Kiwango cha Ada na Ushuru kwa siku (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Gari lenye uwezo wa kubeba uzito chini ya tani 10 | 2,500/ = |
| 2. | Lori lenye uwezo wa kubeba uzito zaidi ya tani 10 | 3,000/= |
| 3. | Gari dogo | 1,000/= |
| 4. | Pikipiki ya magurudumu mawili | 500/= |
| 5. | Pikipiki ya magurudumu matatu | 500/= |
| 6. | Gari dogo la mizigo | 1,500/= |
| 7. | Ada ya kutunza gari lililokamatwa au kuzuiliwa | 20,000/= kwa siku |
| 8. | Ada ya kutunza pikipiki iliyokamatwa au kuzuiliwa | 10,000/= kwa siku |
| 9. | Ada ya kulaza magari kwenye vituo binafsi | 100,000/= kwa mwaka |

SEHEMU YA KUMI NA MBILI

Ada ya Kulaza Magari Maeneo yanayomilikiwa na Halmashauri

| Namba | Aina ya Gari | Ada na Ushuru kwa siku (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Basi kubwa | 3,000/= |
| 2. | Basi dogo | 2,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 3. | Gari dogo la abiria | 1,000/= |
| 4. | Gari dogo la mizigo | 1,500/= |

SEHEMU YA KUMI NA TATU

Ushuru wa Kuingiza Vyombo vya Moto Stendi

| Namba | Aina ya Gari | Kiwango cha Ada na Ushuru kwa siku (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Basi kubwa | 2,500/= |
| 2. | Basi ya kati | 2,000/= |
| 3. | Gari dogo la abiria | 1,500/= |
| 4. | Gari dogo | 1,000/= |
| 5. | Gari la mizigo<br>-tani 1 hadi 3<br>-tani 4 hadi 10 | <br>1,000/=<br>2,500/= |
| 6. | Pikipiki ya magurudumu matatu | 500/= |
| 7. | Pikipiki ya magurudumu mawili | 300/= |
| 8. | Abiria atakayeingia Stendi | 200/= kila anapoingia |

SEHEMU YA KUMI NA NNE

Ada ya Huduma za Usafi

| Namba | Taasisi | Kiwango cha ushuru kwa Mwaka (Shilingi) | Kiwango cha Ushuru kwa Mwezi (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| 1. | Taasisi zote na mashirika | 360,000/= | 30,000/= |
| 2. | Hospitali ya rufaa | 600,000/= | 50,000/= |
| 3. | Viwanda vikubwa | 600,000/= | 50,000/= |
| 4. | Viwanda vya kuoka mikate | 360,000/= | 30,000/= |
| 5. | Hoteli za kitalii | 300,000/= | 25,000/= |
| 6. | Migahawa | 60,000/= | 5,000/= |
| 7. | Useremala | 50,400/= | 4,200/= |
| 8. | Wauza mbao | 60,000/= | 5,000/= |
| 9. | Mashine ndogo za kusaga na kukoboa | 36,000/= | 3000/= |
| 10. | Duka la jumla | 60,000/= | 5,000/= |
| 11. | Duka la rejareja | 25,000/= | 2,000/= |
| 12. | Ghala | 300,000/= | 25,000/= |
| 13. | Viwanda vidogo vya kukamua mafuta | 50,000/= | 5,000/= |
| 14. | Bucha za samaki au nyama | 30,000/= | 2,500/= |
| 15. | Machinjio | 300,000/= | 25,000/= |
| 16. | Baa na mgahawa | 60,000/= | 5,000/= |
| 17. | Mini super market | 60,000/= | 5,000/= |
| 18. | Vilabu vya pombe za kienyeji | 30,000/= | 2,500/= |
| 19. | Nyumba ya kuishi kwa kila kaya | 24,000/= | 2,000/= |
| 20. | Saluni za wanaume na wanawake | 36,000/= | 3000/= |
| 21. | Grosari | 36,000/= | 3000/= |
| 22. | Nyumba za kulala wageni | 600,000/= | 5,000/= |
| 23. | Vituo vya afya na zahanati | 60,000/= | 5,000/= |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 24. | Vituo vya mafuta | 60,000/= | 5,000/= |
| 25. | Maduka ya vifaa vya ujenzi | 60,000/= | 5,000/= |
| 26. | Maduka ya nguo na viatu | 36,000/= | 3,000/= |
| 27. | Maduka ya dawa (Famasi) | 60,000/= | 5,000/= |
| 28. | Maduka ya dawa muhimu | 36,000/= | 3,000/= |
| 29. | Maduka ya mikate na vitafunwa | 25,000/= | 2,000/= |
| 30. | Maduka ya vyombo | 25,000/= | 2,000/= |
| 31. | Maduka ya kuuza magodoro na samani | 30,000/= | 2,500/= |
| 32. | Maduka ya kuuza spea za magari, pikipiki na baiskeli | 60,000/= | 5,000/= |
| 33. | Maduka ya kuuza shajala na kudurufu | 60,000/= | 5,000/= |
| 34. | Maduka ya kuuza vipodozi | 36,000/= | 3,000/= |
| 35. | Maduka ya kuuza simu au saa | 36,000/= | 3,000/= |
| 36. | Mama na Baba Lishe | 30,000/= | 2,500/= |
| 37. | Mgahawa | 60,000/= | 5,000/= |

SEHEMU YA KUMI NA TANO

Ushuru wa Soko kwa Mazao au Bidhaa zitokanazo na Mazao

| Namba | Aina ya Bidhaa | Kiwango cha Ada na Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Mahindi | 1,000/= kwa kila gunia. |
| 2. | Maharage | 1,500/= kwa kila gunia |
| 3. | Muhogo | 500/= kwa kila gunia |
| 4. | Mtama | 1,500/=kwa kila gunia |
| 5. | Mpunga | 1,500/=kwa kila gunia |
| 6. | Dagaa | 1,500/=kwa kila gunia |
| 7. | Samaki | 3,000/= kwa tenga kubwa na 1,500 /= kwa tenga dogo |
| 8. | Vitunguu | 1,500/= kwa kila gunia |
| 9. | Alizeti | 1,000/= kwa kila gunia |
| 10. | Kabeji, machungwa, miwa, nanasi, ndizi, parachichi | 7,000/= kwa kila tani moja |
| 11. | Viazi | 1,500/= kwa kila gunia |
| 12. | Hoho | 500/= kwa kila gunia |
| 13. | Karanga | 2,500/= kwa kila gunia |
| 14. | Njegere maganda | 1,000/= kwa kila gunia |
| 15. | Pumba za mpunga | 500/= kwa kila gunia |
| 16. | Mashudu ya Alizeti | 1,000/= kwa kila gunia |
| 17. | Nyanya | 500/= kwa kila tenga |
| 18. | Mchele | 1,000/= kwa kila gunia au kilo mia moja |
| 19. | Unga | 500/= kwa kila gunia au kila roba au kilo mia moja |

SEHEMU YA KUMI NA SITA

Ada ya Shughuli za Burudani, Utamaduni, Sanaa na Matangazo

| Namba | Aina ya Huduma | Kiwango cha Ada au Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Washereheshaji | 50,000/= kwa tukio |
| 2. | Wapambaji wa kumbi za burudani, harusi, sherehe za jikoni, sherehe za kuanga binti na nyinginezo | 50,000/= kwa tukio |
| 3. | Mpiga muziki (D.J) | 50,000/=kwa tukio |
| 4. | Wamiliki wa kumbi mbalimbali | Ukumbi unaochukua watu 100-200 shilingi 20,000 /=, ukumbi unaochukua watu 300-500 ni shs. 40,000/= kwa kila siku |
| 5. | Matangazo ya barabarani ya sherehe | 50,000/= kwa moja kwa siku |
| 6. | Wapishi wa vyakula | 50,000/= kwa tukio na kwa mpishi moja |
| 7. | Picha jongevu na mnato | 30,000/= kwa tukio moja kwa moja |
| 8. | Matangazo ya kuuza bidhaa zinazopungua bei | 40,000/= kwa tangazo |
| 9. | Maombi ya kibali cha kufanya tiba za jadi | 20,000/= kwa siku |
| 10. | Matamasha | 100,000/= kwa tamasha |
| 11. | Fete na bahati nasibu | 20,000/= kwa siku |
| 12. | Mnada | 40,000/= kwa mnada |
| 13. | Kupiga muziki ukumbi mkubwa | 100,000/= kwa siku |
| 14. | Kupiga muziki ukumbi mdogo | 40,000/= kwa siku |
| 15. | Matangazo ya biashara kwa kutumia vipaza sauti au vipeperushi na au fani za sanaa | 30,000/= kwa siku |
| 16. | Udhamini wa vipindi, filamu na tamthilia | 755,000/= kwa dakika 30 hadi 35 |
| 17. | Taarifa ya Habari | 2,500,000/= kwa siku 30 |
| 18. | Maandishi kupita sauti | 10,000/= kwa sekunde 60 |
| 19. | Picha | 300,000/= kwa sekunde 60 |
| 20. | Picha | 1,000,000/= kwa siku 7 |
| 21. | Mahojiano | 250,000/= kwa dakika 30 |
| 22. | Matangazo ya makampuni mbalimbali asubuhi,mchana na jioni | 3,000,000/= kwa sekunde 60 |

SEHEMU YA KUMI NA SABA

Ada za Ukataji Barabara

| Namba | Aina ya ukataji Barabara | Ukubwa | Gharama (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| 1. | Barabara ya lami | Mita moja | 200,000/= |
| 2. | Barabara ya changarawe | Mita moja | 80,000/= |
| 3. | Barabara ya vumbi | Mita moja | 30,000/= |
| 4. | Ada ya uzio[inalipwa kila baada ya miezi mitatu] | Mita moja ya mraba | 3,000/= |

SEHEMU YA KUMI NA NANE

Ada za Usajili wa Teksi

| Namba | Aina ya Chombo cha Usafiri | Ada (Shilingi) | Muda |
|---|---|---|---|
| 1. | Teksi | 100,000/= | Kwa kila mwaka |

SEHEMU YA KUMI NA TISA

Ushuru wa Mazao ya Misitu

| Namba | Aina zote za mazao ya misitu | Kiwango cha ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Aina zote za mazao ya misitu | Asilimia tano (5%) ya bei ya kununulia |

SEHEMU YA ISHIRINI

Ushuru wa Mazao ya Uvuvi

| Namba | Aina | Uzito | Kiasi cha ushuru kwa siku (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| 1. | Samaki | Kilo 1 | 15/= |

SEHEMU YA ISHIRINI NA MOJA

Ushuru wa Kupakia na Kushusha Mazao

| Namba | Aina | Uzito | Kiasi cha ushuru kwa siku (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| 1. | Mazao | Tani 1 | 3,000/= |

SEHEMU YA ISHIRINI NA MBILI

Ada ya Minara ya Simu

| Namba | Aina ya Ada | Kiasi cha Ada kwa Mwaka (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Mmiliki wa mnara wa simu | 100,000/= |
| 2. | Mmiliki lilikosimikwa bango la Tangazo kwenye eneo la Halmashauri | 10,000/= kwa mita moja ya mraba |

SEHEMU YA ISHIRINI NA TATU

Ushuru kwenye Vivutio vya Utalii

| Namba | Aina ya ushuru | Kiasi cha ushuru kwa siku (shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Vivutio vya utalii vya ndani | 500/= kwa Mtoto |
| 2. | Vivutio vya utalii wa ndani | 1,000/= kwa Mkubwa |
| 3. | Vivutio vya utalii kwa raia wa kigeni | 1,500/= kwa Mtoto |
| 4. | Vivutio vya kitalii kwa raia wa kigeni | 3,000/= kwa Mkubwa |

SEHEMU YA ISHIRINI NA NNE

Ada ya Ujenzi wa Vituo vya Kuoshea Vyombo vya Moto
na Viwanda vya Kufyatua Tofali

| Namba | Sehemu husika | Ada kwa Mwezi (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Maeneo ya katikati ya Manispaa | 100,000/= |
| 2. | Nje ya maeneo ya katikati ya Manispaa | 50,000/= |
| 3. | Viwanda vikubwa vya kufyatua tofali | 100,000/= |
| 4. | Viwanda vidogo vya kufyatua tofali | 50,000/= |

SEHEMU YA ISHIRINI NA TANO

Ada ya kuingiza kontena kwenye eneo la Halmashauri

| Namba | Ukubwa wa kontena | Kiasi kwa tani (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Tani 3 hadi 10 | 50,000/= |
| 2. | Tani 11 hadi 20 | 100,000/= |
| 3. | Tani 21 hadi 30 | 150,000/= |
| 4. | Tani 30 na kuendelea | 300,000/= |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 15)*

FOMU YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ........................................................................ nakiri KWA HIARI YANGU MIMI MWENYEWE mbele ya........................................................... ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa kwamba Tarehe ..........ya Mwezi .................. Mwaka................ nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya aya ya ……..ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Manispaa ya Iringa ya Mwaka 2023.

Hivyo, kwa kuzingatia masharti ya sheria husika, nipo tayari kulipa kiasi cha ada au ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU.

Leo tarehe …………………..ya Mwezi …………… Mwaka …………………
Jina: ………………………………………….
Saini: …………………………….

MBELE YA:
Jina: ……………………………………
Wadhifa: ……………………………….
Saini: ………………………………..
Tarehe: ……………………………

Nembo na Chapa ya Halmashauri yaManispaa ya Iringa imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa na Mkutano wa Baraza la Madiwani wa Halmashauri ulioitishwa na kufanyika tarehe 28 Januari, 2022 na ulibandikwa mbele ya:-

KASTORI G. MSIGALA,
*Mkurugenzi,*
*Halmashauri ya Manispaa*
*Iringa*

IBRAHIM A. NGWADA,
*Meya*
*Halmashauri ya Manispaa*
*Iringa*

**L.S**

NAKUBALI,

Dodoma,
30 Novemba, 2023

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (Mb.),
*Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI*,